Scalabrini Centre of Cape Town

UPDATED: SEPTEMBER 2023

# NITAANZAJE KUTUMA OMBI LA KUTAFUTA KIMBILIO?

Hati hii ni ya kuwasaidia watu kuelewa mfumo wa kutafuta kimbilio nchini Afrika Kusini. Tafadhali kumbuka hati hii ni ya mwongozo pekee. Si ya ushauri wa kisheria. Maelezo haya yanaweza kubadilika. Tembelea www.scalabrini.org.za/information-about-asylum-in-south-africa kwa maelezo yaliyosasishwa. Scalabrini Centre of Cape Town (Kituo cha Scalabrini cha Cape Town ) haitawajibika kwa hatua zinazochukuliwa kwa kutumia maelezo kwenye hati hii.



## DOKEZO MUHIMU

**Ni muhimu sana kusajiliwa nchini Afrika Kusini. Hati za usajili zinakulinda kutokana na kukamatwa na kufukuzwa nchini na huhakikisha unapata huduma fulani. Watu wanaotoroka migororo au mateso wanapaswa kutuma maombi ya kutafuta kimbilio nchini Afrika Kusini. Kwa kufanya hivyo, unaiomba serikali ya Afrika Kusina ikupe ulinzi kwa njia ya usajili wa mkimbizi au anayetafuta kimbilio. Utaratibu huu unaweza kuchukua muda mrefu. Ni muhimu utoe maelezo ya kweli na sahihi katika utaratibu huu wote. Ikiwa huzungumzi vizuri lugha ya Kiingereza, ni muhimu sana uombe huduma ya mtafsiri ili akusaidie unapokuwa katika Ofisi ya Mapokezi ya Wakimbizi (Refugee Reception Office). Hati hii itatafsiriwa kwa lugha zifuatazo: Nenda kwenye www.scalabrini.org.za/information-about-asylum-in-south-africa ili uone hati hii katika lugha nyingine.**

### HATUA YA 1



CHAGUA NI OFISI GANI YA MAPOKEZI YA WAKIMBIZI (RRO) AMBAYO UNGEPENDA KUTUMA OMBI LAKO

### HATUA YA 2



WATU KUTOKA NCHI MBALIMBALI WANAHITAJI KWENDA KWENYE OFISI YA MAPOKEZI YA WAKIMBIZI KATIKA SIKU TOFAUTI. TUMIA JEDWALI LETU KATIKA UKARASA UNAOFUATA ILI KUJUA SIKU YAKO YA KWENDA.

### HATUA YA 3



NENDA MOJA KWA MOJA KWENYE OFISI YA MAPOKEZI YA WAKIMBIZI KATIKA SIKU HIYO. UKIWA HUKO, WEKA MIADI YA KUTUMA OMBI LA KUTAFUTA KIMBILIO.

### HATUA YA 4



HUDHURIA MIADI YAKO ILI BIOMETRIKI NA DATA YAKO IREKODIWE.

### HATUA YA 5



BAADA YA MIADI YA KWANZA, UTAHUDHURIA MIADI YA PILI AMBAPO UTAHOJIWA NA AFISA WA UBAINISHAJI WA HALI YA UKIMBIZI. KISHA UTAJULISHWA UAMUZI KUHUSU OMBI LAKO.

### HATUA YA 6



MARA UNAPOPEWA HALI YA KIMBILIO, UNAWEZA KUPATA VIZA YAKO YA KIMBILIO KWA KUFUATA UTARATIBU WA KUTUMA OMBI MTANDAONI

PATA MAELEZO ZAIDI KWENYE UKURASA UNAOFUATA

Scalabrini
Centre of Cape Town

**UPDATED: SEPTEMBER 2023**

## HATUA YA 1 — CHAGUA AFISI YA MAPOKEZI YA WAKIMBIZI YA KUTUMA OMBI NA WAKATI WA KUITEMBELEA

Unaweza tu kutuma ombi la kutafuta kimbilio nchini Afrika Kusini ikiwa kwa sasa uko ndani ya mipaka ya Afrika Kusini. Unapaswa kutuma ombi la kutafuta kimbilio haraka iwezekanavyo. Ili kutuma ombi la kutafuta kimbilio nchini Afrika Kusini, utaanza utaratibu huu kwa kutembelea Ofisi ya Mapokezi ya Wakimbizi ambapo ungependa kutuma ombi.

Chaguo zako ni:

- Durban Refugee Reception Office
- Pretoria (Desmond Tutu Refugee Reception Office)
- Musina Refugee Reception Office
- Gqeberha Refugee Reception Office (formerly Port Elizabeth)
- Cape Town Refugee Reception Office




Angalia jedwali lililo hapo chini ili ujue siku unayoweza kutembelea Ofisi ya Mapokezi ya Wakimbizi.
Hii inategemea nchi uliyotoka.

| SIKU | NCHI | LUGHA |
|---|---|---|
| **JUMATATU** | Angola, Botswana, DRC, Tanzania, Lesotho, Madagascar, Malawi, Mauritius, Mozambique, Namibia, Seychelles, Zimbabwe, Swaziland, Egypt, Algeria, Pakistan, India, China | French, Swahili, Lingala, Tshiluba, Shona, Chichewa, Portuguese, Arabic, Bangali, Urdu, Gujarat, Punjabi, Hindi, Tsonga |
| **JUMANNE** | Angola, Botswana, DRC, Lesotho, Madagascar, Malawi, Mauritius, Mozambique, Namibia, Seychelles, Zimbabwe, Swaziland, Egypt, Algeria, Pakistan, India, China | French, Swahili, Lingala, Tshiluba, Chichewa, Portuguese, Arabic, Bangali, Urdu, Gujarat, Punjabi, Hindi, Ndebele |
| **JUMATANO** | Ethiopia, Burundi, Rwanda, Uganda, Eritrea, Kenya | Amharic, Hadiya, Kambati, Oromo, Swahili, French, Kirundi, Kinyarwanda, Tigrinya, Luganda, |
| **ALHAMISI** | Somalia, Cameroon, Senegal, Eritrea, Ethiopia, Ghana, Burundi | French, Wolof, Swahili, Lingala, Twi, Somali, Amharic, Hadiya, Oromo, Tigrinya, Kambata, Kirundi |
| **IJUMAA** | Somalia, Senegal, China<br><br>French, Swahili and Lingala speakers | French, Swahili, Mandarin, Lingala, Somali, Wolof |

Scalabrini Centre of Cape Town

## HATUA YA 2 — NENDA KWENYE OFISI YA MAPOKEZI YA WAKIMBIZI ILI UWEKE MIADI YAKO

Mara unapotambua Ofisi ya Mapokezi ya Wakimbizi ambayo ungependa kutuma ombi na unapojua siku ya kutembelea Ofisi hiyo ya Mapokezi ya Wakimbizi, nenda moja kwa moja huko ili uweke miadi yako ya kutuma ombi la kutafuta kimbilio.

Beba kitambulisho cha nchi yako au kibali cha Section 23 (viza ya muda ya mtafuta kimbilio).
Ikiwa hauna hati hizi, unapaswa kupata hati ya kiapo inayotaja wakati ulipowasili nchini na uende nayo kuweka miadi yako.

**Tunakuhimiza uweke vizuri kipande cha karatasi utakachopewa unapoweka miadi yako. Tunakuhimiza pia ujipige picha ukiwa katika Ofisi ya Mapokezi ya Wakimbizi, kama uthibitisho.**

## HATUA YA 3 — HUDHURIA MIADI YAKO

Rudi kwenye Ofisi ya Mapokezi ya Wakimbizi mnamo tarehe uliopangiwa miadi yako.

Katika miadi ya kwanza, maafisa watarekodi biometriki na data yako. Hii inamaanisha kwamba watarekodi alama za vidole vyako na maelezo yako binafsi.

**Kisha utapangiwa miadi ya pili**


Katika miadi hii ya pili, utahojiwa na Afisa wa Ubanishaji wa Hali ya Ukimbizi (RSDO). Kabla ya kuhojiwa, RSDO atakuelezea utaratibu huo. Wakati wa mahojiano, RSDO anapaswa kukuuliza sababu za kutoroka nchi yako na kwa nini inaweza kuwa hatari kurudi huko. Anaweza kuomba uthibitisho au ufafanuzi wa maelezo unayomwambia.

**Kisha utajulishwa uamuzi kuhusu ombi lako la kutafuta kimbilio.**

## HATUA YA 4 — BAADA YA MAHOJIANO YAKO, UNAWEZA KUTUMA OMBI MTANDAONI

Baada ya miadi yako na Afisa wa Ubainishaji wa Hali ya Ukimbizi (RSDO), utapewa nambari ya kumbukumbu. Kwa kutumia nambari hii ya kumbukumbu, unaweza kutuma ombi la mtandaoni la kibali chako cha kimbiliko ukitumia utaratibu sawa na kutuma barua pepe.

### MFANO WA MAELEZO UNAYOPASWA KUJUMUISHA KWENYE BARUA PEPE YAKO....




Mstari wa mada utaandika nambari yako ya kumbukumbu.

Nambari yako ya Kumbukumbu inaanza kwa herufi tatu. Inaweza kuanza na CTR, MUS , PTA, ECZ au DBN, kisha ikifuatwa na nambari kadhaa.



**Angalia mchoro wetu wenye maelezo kwa utaratibu wa kutuma ombi kupitia barua pepe au utembelee tovuti yetu (scalabrini.org.za/information-about-asylum-in-south-africa)**

**Tunawahimiza watu wote watume maombi wao wenyewe na wafuate utaratibu ulioelezwa hapo juu. Scalabrini Centre of Cape Town inatoa usaidizi mdogo sana inapowezekana kwa watu wanaotumia au wanaotuma maombi ya huduma za mtandaoni za Idara ya Mambo ya Ndani (Home Affairs).**

